

# HALMASHAURI YA MJI WA KONDOA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa Kondoa)

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255 262360313

Barua pepe: [td@kondoatc.go.tz](mailto:td@kondoatc.go.tz)

Tovuti: [www.kondoatc.go.tz](http://www.kondoatc.go.tz)



Mkurugenzi wa Mji  
S.L.P 711,  
KONDOA.

Kumb.NA.KTC/S.20/Vol.II/56

21.03.2018

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kufuatia Halmashauri ya Mji ya Kondoa kupata kibali cha ajira chenye Kumb. NA. CFC 26/205/01"GG"/95 ya tarehe 12 Machi, 2018 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma kuhusu ajira mpya , Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa anatangaza nafasi za kazi na anakaribisha maombi kwa Watanzania wenye sifa za kujaza nafasi kama zilivyoorodheshwa katika tangazo hili:-

### 1:- Mtendaji wa Kijiji Daraja la III (nafasi 11 )

#### 1.1: Kazi na majukumu

- ❖ Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo Kijijini.
- ❖ Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao
- ❖ Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Kijiji
- ❖ Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote za nyaraka za Kijiji
- ❖ Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- ❖ Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Kijiji
- ❖ Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ❖ Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi

#### Sifa za Mwombaji.

- ❖ Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au cha sita na mafunzo ya Astashahada /cheti katika moja ya fani zifuatazo:- Utawala , sheria , Elimu ya Jamii , Usimamizi wa Fedha , Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

Mshahara kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya **Serikali TGS B** kwa mwezi.

**MASHARTI KWA UJUMLA**

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- ii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza ( Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini ( referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma , maelezo , nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa . Viambatanisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea . Picha moja "Passport Size" ya rangi ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- v. Testimonials" **Provisional Results" Statement of Results**" hati matokeo za kidato cha nne na sita ( **FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA**
- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika ( TCU na NECTA)
- vii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua kali za kisheria.
- ix. Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 04 APRILI, 2018**
- x. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kingereza au Kiswahili na yatumwe moja kwa moja kwa njia ya posta kwa kutumia anuani ifuatayo hapa chini:-

**Imetolewa na :-**

**MKURUGENZI MJI,  
S.L.P 711,  
KONDOA**

*Ally*

.....  
**ALLY MWINYIKOMBO  
KAIMU MKURUGENZI MJI  
KONDOA**

